Zakayo, Yule Mfanyabiashara

Kila mtu amekuwa akitoa ushuhuda usiku wa leo, akielezea matukio makubwa sana. Nami kwa kweli ninafurahia mambo hayo. Na imeonekana kana kwamba kila mtu alikuwa na kaucheshi kidogo katika ushuhuda wao.

2 Nami huenda pengine niongezee hili kwa wangu. Kama vile yule bibi mweusi alivyotaka kushuhudia si muda mrefu uliopita, anasema, "Mzee, je! ningeweza kushuhudia?"

Nikasema, "Endelea tu."

3 Naye akasema, "Si—si—sigo vile na—vile napaswa kuwa, na—na mimi—na sigo vile ninavyotaka kuwa," akasema, "bali siko vile nilivyokuwa, pia."

4 Kwa hiyo basi ni karibu kama vile ninavyojisikia miongoni mwa kundi kama hili. Siko vile ninavyopaswa kuwa, wala vile ninavyotaka kuwa, bali, ninajua jambo moja, siko jinsi vile nilivyokuwa. Nami ninakaza mwendo kuifikia ile mede ya Wito mkuu.

5 Najisikia vizuri sana kuwapo hapa. Tumekuwa na mmoja wa nyakati nzuri sana za ushirika pamoja na ndugu zetu, huko kwenye Bonde la Maricopa, majuma haya mawili ya mwisho. Kwa namna fulani nimepwelewa na sauti. Pia tumemwona Baba yetu wa Mbinguni akitufanyia mambo makuu. Nasi tunafanya jambo hili kwa namna fulani kuwafanya watu waombe, na tunatarajia kufikia upeo mkuu uje wakati wa mkutano huu. Wakati . . .

6 Nilisikia kwamba nilikuwa na majaliwa ya kuja kwenye tawi hili, pamoja na rafiki yangu wa thamani, Ndugu Tony. Na nimeuliza mara tatu, usiku wa leo, je! mnalitamkaje jina hilo? Nami ni—siwezi tu kabisa kulipata. Na kwa hiyo ni "Tony" tu, kama hilo ni sawa. Nafikiri sisi hapa hatuna utaratibu sana, hata hivyo, sivyo? Unajua, hilo kwa namna fulani ni la kiungu. Unajua, Biblia ilisema, "Mungu hana umbo." Kwa hiyo hatuna mpangilio wo wote.

7 Tukiona mambo makuu ambayo Baba yetu wa Mbinguni ametufanyia juma hili, tuna furaha kuja huku na kushiriki baraka hizi kwenye tawi hili, na tupate kukutana na baadhi ya ndugu, na ninyi watu kutoka hapa chini katika sehemu hii ya—ya Arizona. Ambapo, sote tunajua, hapa chini, ya kwamba huu ndio mji mkuu. Nimewaambia juma zima ya kwamba Phoenix ulikuwa tu ni vitongoji vya Tucson, daima. Unaona? Hawataliamini jambo hili, lakini tunawakaribisha kwenye ushirika wetu. Hii ni, kwa kuwa tuko juu zaidi. Inawabidi watuangalie kwa juu, unaona, hapa juu Tucson. Na kwa hiyo

ninyi nyote mje huku, nasi tutaenda huko na kuutembelea Phoenix sasa, juma lijalo, ama mwishoni mwa juma hili, kwa ajili ya wakati huu wa ushirika kule juu.

8 Tulikuwa na jambo kuu lililotukia kabla tu sijatoka kuja kwenye safari hii. Ningetaka tu kuchukua muda mfupi kwa kuwa nafikiri lingekuwa ni jambo linalofaa. Mimi . . .

9 Katika kusafiri miaka hii yote na kujaribu kusimama kati ya pengo, madhehebu mbalimbali na watu, Wakristo Wafanyabiashara kwa namna fulani walikuwa ni oasisi ndogo kwangu, kuamini ya kwamba Mungu aliyafanya mataifa yote kwa damu moja. Nami—ninaamini hivyo. Ninaamini ya kwamba watu wake wamo katika makanisa yote. Kama Yeye kweli ni Mungu, Yeye ni Mungu wa jamii yote ya binadamu, Mungu wa uumbaji. Naye bila shaka anaweza . . . Angalia huko nje kwenye majangwa na milima, unaweza kuona yale anayopenda, kwa maana anajionyesha katika uumbaji Wake. Nasi tunaweza kuona ya kwamba kuna Mungu. Na watu hawa, Wafanyabiashara wa Full Gospel, wakati ninapokwenda kwenye matawi yao, nikizungumza kwa niaba yao, basi inanipa nafasi kuweza kuyazungumzia makundi yote mbalimbali, kwa pamoja.

10 Niliitwa kwenda, kile tungeweza kukiita kwa msemo wa kidunia, kumdokoa Demos Shakarian. Unajua jinsi—jinsi hiyo ilivyo kazi ngumu. Lakini nilikuwa huko Cincinnati siku chache zilizopita, naye Dada Shakarian, ninavyofahamu mimi, alifanyiwa upasuaji. Ndugu Miner Arganbright, mmoja wa maafisa, alinipitia na kusema, "Jiunge nami twende Cincinnati kwa gari."

11 Nikasema, "Nina mamia ya watu waliolala hapa, kutoka kote ulimwenguni, wamelala kwenye hospitali hizi na vyumba, wakiningojea niwaombee. Wamekuwa wakingojea mazungumzo ya faragha, labda wengine kufikia muda wa miaka miwili ama mitatu, wamekuwa wakingoja, na hatimaye wakafika hapa."

Naye akasema, "Vema, tukimbie huko tu kwa dakika chache."

12 Nikasema, "Vema, kiamshakinywa ni saa ngapi?" Ni kama maili mia moja na ishirini, nakisia, kutoka mahali ninapoishi.

Naye akasema, "Vema, kinaanza kwenye kama saa mbili."

13 Nikasema, "Vema, ngoja nikwambie. Tutapanda twende kule basi, saa kumi hivi, na kufika kule kwa ajili ya kiamshakinywa. Nitaharakisha kurudi mara moja."

14 Ndipo nilipofika kule, Ndugu Shakarian hakuwako. Ndipo nikaingia. Kasema, "Kile hasa tulichokuwa tukitafuta!" Na kwa hiyo usiku huo, kwenye wakati fulani, ilinibidi nirudi nyumbani.

15 Kwenye wakati huo, kulikuwako na mhudumu Mbaptisti aliyekuwa ndiyo kwanza amelala kabisa kwenye bega la Billy,

mwanangu, na kusema, “Hufahamu, bwana.” Akasema, “Mke wangu anakufa.”

16 Naye akasema, “Vema, bwana, baba atakaporudi.” Kasema, “Tunawajibika kwa watu hawa, kwamba tuje.”

17 Unajua, kwenye mstari wa maombi, mara nyingi, tukipitia, na labda tukifanya maombi. Lakini wewe. . .Na mara nyingine ugonjwa fulani una mambo mazito zaidi kuliko hivyo. Unaona, Mungu huponya kwa masharti, na huenda kukawa kuna jambo fulani katika maisha ya mtu huyo. Na sijali ni madawa mangapi daktari angewapa, hawatapona kamwe mpaka jambo hilo limewekwa sawa.

18 Kama ungalienda kwenye ofisi ya daktari fulani na kumwambia kwamba wewe ulikuwa mgonjwa, na ukamwambia dalili zako, naye alikuwa ana haraka, labda angekupa maelekezo mafupi chenye kituliza maumivu fulani ndani yake, cha namna fulani, asprini chache. Huyo daktari anajaribu tu kukuondoa, kwenye wakati huo tu, kwa maana hana wakati. Daktari mzuri wa kweli, kabla hajakupa hiyo dawa, angebaini ugonjwa huo, kikamilifu, mpaka aone kuna shida gani, ndipo akupe dawa.

19 Na mara wakati mwingine tunapata watu wanaopitia kwenye mistari hii ya maombi, huko nje katika mataifa mbalimbali, na wanakimbia tu kuja na kufikiri ya kwamba Bwana anapaswa kuwaponya papo hapo. Lakini labda kuna jambo fulani katika shida hiyo, nasi tunaketi mbele za Bwana mpaka anapolifunua hilo, kwamba ni jambo gani. Kuna jambo linalopaswa. . .Kuna ninii—kuna sababu kwa kila kitu. Nawe huna budi kugundua sababu hiyo, kwanza, na ndipo unaweza kuona ni jambo gani la kushughulikia.

20 Basi kijana huyu akaendelea kusisitiza. Nami nikaingia kesho yake asubuhi kama saa nane usiku. Na yapata kama saa kumi na moja, mwanangu akanipigia simu, na kusema, “Je! unamjua msichana mmoja anayeitwa Jean Dyer?”

Nikasema, “Jean Dyer, linasikika kama ninamfahamu.”

Akasema, “Yeye alisema alikuwa akikupigia piano.”

21 “Loo,” nikasema, “huyo siye Dkt. Dyer, yule daktari mpasuaji hapa, mpasuaji anayejulikana sana Louisville?”

22 Kasema, “Naam—naam ndiye huyo. Vema, binti yake Jean anakufa huko katika Hospitali ya Mtakatifu Edwards katika . . . ama Hospitali ya Mtakatifu Anthony, hasa, huko Louisville.” Akaongezea kusema, “Mume wake amekaa kwenye vipandio siku nzima.”

“Vema,” nikasema, “vema, nitajaribu kujipenyeza kwenye hilo leo.”

23 Kasema, “Sasa, huyo msichana hajui kwamba ana kansa. Usimwambie.”

24 Kwa hiyo, hatimaye, siku hiyo, ndipo nilipofika kwenye hicho chumba; ni kijana mwanamke mzuri.

25 Alikuwa amenipigia piano, katika ninii . . . nilipokuwa kule kwenye jumba la mikutano, ambako niliwaona watu wa Ndugu Allen, waliopo hapa usiku wa leo. Ndugu Allen alikuwa ndiyo kwanza aondoke kwenye jumba lilo hilo la mikutano huko Lousiville. Hilo ni Jumba la Kumbukumbu la Mikutano. Naye Jean Dyer alikuwa ndiye mpiga piano katika kanisa liitwalo Mlango Uliofunguliwa, lile sinagogi la zamani. Na kwa hiyo yeye alikuwa ameona mambo makuu ambayo Bwana Mungu alikuwa amefanya. Alimwambia baba yake.

26 Baba yake alisema tu, "Hiyo ni saikolojia tupu. Mtu huyo anasoma tu akili za watu. Kuna . . . Amekisia tu hayo."

27 Akasema, "Baba, haiwezi ikawa ni kukisia kila wakati." Unaona? Akasema, "Haiwezekani kabisa."

"Vema," akasema, "Jean, sahau upuuzi huo."

28 Naye alikuwa ameposwa na mvulana mzuri aliyekuwa akisoma kwenye ile seminari ya Kibaptisti wakati huo. Alifunga ndoa na kuhamia Rockford, Illinois, yalikokuwa makazi ya mvulana huyu. Na kwa namna moja ama nyingine alikazana kushikilia ushuhuda wake. Lakini huyo mvulana alitoka akaingia katika kazi ya kidunia, na baada ya kitambo kidogo karibu amwache Bwana.

29 Msichana huyo alikuwa na u—ugonjwa wa kike. Akaenda nyumbani kwa baba yake. Baba yake alijua alihitaji upasuaji. Alikuta ndani yake kile kinachoitwa . . . Na sijui jina lake la kitabibu, lakini, sababu ninajua kuna baadhi ya madaktari walioketi hapa sasa. Kwa hiyo, iliitwa, kitu kama uvimbe wa chokoleti. Na ni ninii . . . Ndani yake, wakati alipouondoa, hapana budi alitapanya sehemu za huo. Na seli hizo zilikuwa ni za kufisha. Na wakamshona, wakamfanyia eksirei na kumtibu kwa mionzi.

30 Kwa hiyo, alipofika nyumbani, aliendelea kupata maumivu na taabu.

31 Mwaka mmoja baadaye, alirudi akatolewe tumbo lote la uzazi. Basi walipoondoa hizo ogani, walikuta kansa ilikuwa imeingia kwenye utumbo mpana na kujizungushia mle. Hakukuwa na kitu kingaliweza kufanyika. Walijaribu kumfanyia eksirei tena. Haikufaa kitu. Kwa hiyo walimpeleka tu hospitalini na kumwambia alikuwa tu na ugonjwa mbaya sana wa kike, nao wanajaribu kuutibu. Wakati msichana huyo alikuwa anakufa.

32 Mumewe alijua jambo hilo. Kwa hiyo alikuwa amekuja na kuchukua baadhi ya vitabu vyangu, ambavyo Jean alikuwa amevisoma. Na kwa hiyo akaanza kuja hospitalini, akimsomea.

33 Na wakati tulipokwenda kumwombea, huyo msichana alikuwa akiniambia juu ya hayo. Nikasema, "Jean. . . " Yeye ni mvulana mzuri. Nami sikutaka kumwacha. . .Ninaitunza ile siri, maana nilijua ya kwamba—ya kwamba yeye. . . Hakujua alikuwa na kansa. Na kwa hiyo, siku mbili baadaye, walikuwa wamfanyie upasuaji wa—wa utumbo mpana. Kwa hiyo kumchukua. . .

34 Kabla hawajamchukua msichana huyo, vema, walinipa ruhusa ya kuja na kuomba pamoja naye. Nilimpata kwenye chumba kimoja. Na mara nilipofika. . .Kulikuwako na nesi asiyeamini kwenye zamu; kulikuwako na manesi watatu, zamu za saa tatutatu. Na mara tu tulipoweza kumwondosha yule nesi, na kumtoa kwenye kile chumba, kusudi ono litimie, nasi tukaomba pamoja naye kwa muda kidogo pale, ndipo nikamwona. Yeye ana nywele nyeusi. Ana umri wa miaka kama thelathini na sita tu. Nywele nyeusi zilizokuwa zimeingia mvi. Katika hilo ono alikuwa amesimama.

35 Nikasema, "Jean, sasa hebu sikiliza. Nitakuwa mwaminifu sana kwako." Nikasema, "Umekuwa mikutanoni kwa muda mrefu vya kutosha kujua ya kwamba nisingekwambia jambo lo lote katika Jina la Bwana lisipokuwa ndivyo kweli lilivyo." Nikasema, "Sasa Jean, una kansa."

Akasema, "Nilituhumu jambo hilo, Ndugu Branham."

36 Ndipo nikasema, "Upasuaji huo, kesho kutwa, ni wa utumbo mpana. Lakini, usiwe na wasiwasi. Nimeona, kutoka kwa Bwana, utapona." Naye alifurahi tu. Kwa hiyo nikaenda nyumbani.

37 Ndipo kesho yake walikuwa wanaenda kuninii, kesho kutwa yake, hasa, walikuwa wanaenda kumpeleka akafanyiwe upasuaji wa utumbo mpana asubuhi hiyo, nao iliwabidi ku—iliwabidi kungojea kwa dakika chache baada ya kumwandaa, na kadhalika, na akiwa tayari kwenda. Na kulikuwako na. . .Alishikwa na haja ya kawaida ambayo wanadamu wanapaswa kuwa nayo katika wakati huo, nao wakampeleka msalani, naye alijisaidia kawaida kabisa. Daktari alishangazwa sana. Akamfanyia uchunguzi tena. Kesho yake asubuhi. . . Walimwachilia aondoke, wakafutilia mbali upasuaji. Dkt. Hume, mtaalamu hodari sana, mpasuaji, rafiki yangu, alikuwa yuaenda kumfanyia upasuaji.

38 Na kesho yake asubuhi alijisaidia kawaida kabisa tena. Ndipo baba yake, Dr. Dyer, akanipigia simu. Na huku akilia kwa kwikwi, alisema, "Ndugu Branham, nimekuwa mkosoaji wa yale unayosema." Akasema, "Bali sasa mimi ni mwaminio, ya kwamba Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo angali anaishi."

39 Yeye daima alikuwa ni Mungu, anadumu kuwa Mungu. Nasi tunajua ya kwamba Yeye ni mkuu tu hapa Tucson kama alivyo mahali po pote, kwa kuwa Yeye yupo mahali pote, ana nguvu

zote, na hana kikomo, na tunajua ya kwamba anaweza kufanya mambo yote.

40 Sasa, ili nisiwacheleweshe sana. Kwa kawaida, ni kwa nadra sana, wakati mimi . . . Kama nilikuwa nikienda kuhubiri, loo, ningehakikisha nimewatoa katika muda wa saa sita. Hayo ni mahubiri mafupi. Lakini sitafanya hivyo usiku wa leo. Nina ibada nyingi kesho usiku, usiku ufuatao, na kuendelea. Tutajaribu . . .

Ninajiandaa kwenda katika nchi za ng'ambo tena, Bwana akipenda, mara moja.

41 Ninataka kuwaambia watu wote hapa, marafiki, ya kwamba labda baadhi yenu nimekutana nanyi hapo awali, na labda kuna wengi hapa ambao sijakutana nao hapo kabla. Ninawasalimuni katika Jina la Bwana wetu Yesu, Mwana wa Mungu. Amani Yake na iwe pamoja nanyi daima.

42 Na nikizungumza wakati fulani katika matawi haya, kwa namna fulani inawafanya watu kuninii . . . kama vile kwa ndugu zangu wahudumu hapa, kusema . . .

43 Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, kasema, "Billy, vema, kwa nini—kwa nini unashikamana na kundi hilo la wafanyabiashara?" Kasema, "Nilidhani wewe ulikuwa ni mhubiri."

"Loo," nikasema, "Mi—mimi ni mfanyabiashara."

Akasema, "Ati mfanyabiashara?"

Nikasema, "Hakika."

Kasema, "Si—si—sikujua hilo."

Nikasema, "Naam, mimi ni mfanyabiashara."

Kasema, "Uko kwenye biashara ya aina gani?"

44 Nikalisema haraka, kusudi yeye . . . Nikasema, "Niko katika ile dhamana ya Uzima."

Akasema, "Ati nini?"

Nikasema, "Ile Dhamana ya Uzima."

Akasema, "Una maana gani?"

Nikasema "Dhamana ya Uzima wa Milele."

45 Sasa, kama ye yote wenu ninyi watu angetaka kuzungumza juu ya hati ya bima na mimi, nitafurahia kukuona mara baada ya ibada. Mimi—niko hapa kwa ajili ya biashara.

46 Ninamkumbuka rafiki yangu mmoja, jina lake lilikuwa ni Snyder. Tulisoma pamoja. Na sasa, bima, nina rafiki aliye katika biashara ya bima. Nina ndugu aliye kwenye biashara ya bima, lakini kwa kweli mimi—mimi sina bima yo yote. Kwa hiyo huyu Wilmer Snyder, rafiki yangu, rafiki wa ujanani, alinijia mimi si muda mrefu uliopita, naye akasema, "Aisee, Billy," kasema, "ningetaka kuzungumza na wewe kuhusu bima fulani."

47 Nikasema, "Sasa, Wilmer." Nikasema, "Hebu nikwambie. Hebu na tuzungumze juu ya kuwinda."

Akasema, "La. Ninataka kuzungumza juu ya bima."

48 Vema, ilibidi nimtamkie hilo kwa haraka, pia. Nikasema, "Nina dhamana." Si bima ; dhamana, unaona.

49 Ndipo mke wangu akaniangalia, kana kwamba kusema, "Mbona, ewe maskini mhadithiaji." Yeye akijua sikuwa na bima yo yote.

50 Na huyo mtu akasema, "Loo, samahani, Billy." Kasema, "Hiyo ni kweli. Ndugu yako ni wakala. Ninamjua Jesse."

Basi nikasema, "Vema," nikasema, "si na yeye hasa."

Akasema, "Una bima ya aina gani?"

Basi nikasema, nikasema, "Nina Uzima wa Milele."

Akasema, "Ati nini?"

Tena nikasema, "Ule Uzima wa Milele."

51 "Vema," akasema, "sidhani nimewahi kusikia juu ya kampuni hiyo." Kasema, "La. Ni ngeni."

52 Ndipo nikasema, "Ni hivi, Wilmer." Nikasema, "Ni dhamana iliyobarikiwa, Yesu ni wangu. Loo, ni onjo la awali la utukufu wa Kiungu la jinsi gani! Mimi ni mrithi wa wokovu, niliyenunuliwa na Mungu, nimezaliwa kwa Roho Wake, nimeoshwa katika Damu Yake."

53 Akasema, "Hiyo ni nzuri sana, Billy, bali hiyo haitakuzika nje huku makaburini."

54 Nikasema, "Lakini itanitoa kaburini. Sina ninii—sina sana wasiwasi kuhusu kuingia. Ni suala la kutoka, ndilo ninalowazia."

55 Sasa, kama una wasiwasi wo wote, nitazungumza nawe juu ya jambo hilo. Kwa mazungumzo mafupi—mafupi tu kutoka kwenye Maandiko, ingawa ni wafanyabiashara. Lakini nimejitambulisha kama mfanyabiashara pamoja nanyi.

56 Na wengi wa ndugu zangu wahudumu hapa nje, nimewaona wakiamka, muda mfupi uliopita. Na kwa hiyo labda wakati mwingine, Bwana akipenda, ningetaka kuwa pamoja na kundi hilo na nije niwe na mkutano mzuri wa ushirika pamoja na wahudumu hapa chini. Ninamjua maskini ndugu mmoja hapa. Nilikutana naye. Whittle, ninaamini, ndilo lilikuwa jina lake. Tulikuwa tumetoka wote pamoja, wakati mmoja. Sasa, nilitamka hilo vibaya, pia. Alinijulisha kwamba hayo yalikuwa ni sahihi.

57 Na kwa hiyo jina langu mimi ni Bran-ham, mnajua. Mtu mmoja aliniambia, kasema, "Je! . . . Ndugu Bran-ham, wewe ni wa ukoo wa Ibrahimu?"

Nikasema, "Mwanawe."

58 "'Baba wa mataifa.' Tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni uzao wa Ibrahimu, na warithi pamoja naye kulingana na ile ahadi." Hayo ni Maandiko.

59 Sasa, sina wakati wa kuwashikilia hapa, kuhubiri, kwa maana Ramada wasingewaruhusu kamwe kuichukua tena.

60 Kwa hiyo ninakumbuka wakati nilipokuja kwanza miongoni mwa Wapentekoste, miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa huko Mishawaka. Kulikuwako na makundi mawili yao. Moja liliitwa P.A. la W.; lingine, P.A. la J.C., ninaamini. Nao walikuwa na ninii wao—mkutano wao huko pande za kaskazini, kwa kuwa kulikuwako na ubaguzi, na kwa hiyo ndugu weusi wangeweza kuhudhuria mkutano huo. Niliwaangalia siku nzima, jinsi walivyokuwa wa kipekee, hawana nidhamu ya kanisani tena. Jamani! nilikuwa nimeketi pale, na sisi Wabaptisti, unajua, kwa namna fulani tunajaribu kwenda kikanisa-kanisa kanisani. Lakini jamaa hawa hawakuwa na nidhamu yo yote ya Kibaptisti hata kidogo, wala nidhamu yo yote ya kanisa. Wangekimbia, wapige makelele, wapaze sauti, wageuke kuwa na rangi ya bluu usoni. Basi nikawazia "Jamani, jamani!" Na kwa hiyo nikaanza kuona jinsi walivyokuwa wakifanya makelele.

61 Na kwa hiyo mtu mmoja akasema, "Wahudumu wote, waje jukwaani. Kila mhudumu, haidhuru ni wa madhehebu gani, panda huku jukwaani kwa ajili ya jioni hii." Tulikuwa kama watu mia tano tumeketi jukwaani. Kwa hiyo akasema, "Simama tu na utaje jina lako, uketi chini." Ni—nikaja, zamu yangu. Ni—nikataja jina langu, nikaketi chini. Wakaendelea. Baada ya kitambo kidogo, walikuwa na mtu fulani . . . Walikuwa na baadhi ya wahubiri wazuri siku hiyo. Loo, walikuwa ni wasomi kwelikweli, na watu wanyofu. Nami nilijua sikuwa na shughuli yo yote pale, nikiwa na elimu yangu ya darasa la saba, kusimama mbele ya jamaa hao, wakati walikuwa wanakwenda kuzungumza juu ya thiolojia.

62 Lakini niliwazia, "Vema, kwa ajili ya mkutano wa jioni hii, bila shaka watakuwa na mhubiri wao muhimu sana kwa jioni hii."

63 Na kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, wakasema mzee fulani ataenda kuzungumza. Ilikuwa ni mzee mmoja mweusi, aliyetokea. Naye alionekana kuwa ana umri wa miaka kama themanini na mitano. Naye alikuwa amevaa moja ya yale ninii marefu ya zamani, yale tuliyokuwa tunayaita huko kusini, makabuti ya mhubiri, unajua; kwa namna fulani fesheni ya mkia wa mbayuwayu, unajua, milia ya kwenda juu na kushuka chini. Mzingo mdogo wa nywele nyeupe kukizunguka kichwa chake. Naye ilimbidi amwongoze maskini mzee huyo kumtoa, alikuwa ni mzee sana.

64 Naye akatoka pale na kuchukua somo lake kutoka katika Ayubu. Akasema, "'Ulikuwa wapi nilipouweka msingi wa nchi?

Niambie ilikazwa juu ya nini.'" Kasema, "'Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha,'" kasema, "'ulikuwa wapi?'" Mungu akiwa anazungumza na Ayubu.

65 Vema, ndugu wote siku hiyo walikuwa wakihubiri juu ya Maisha ya Kristo, na kule kuja kwa Yohana, wakiunganisha pengo, na kadhalika, kielimu sana.

66 Lakini mzee huyu hakuhubiri juu ya cho chote kilichokuwa kikiendelea hapa chini duniani. Alimchukua huko nyuma kama miaka milioni kumi kabla ulimwengu hata haujapata kuumbwa. Kisha akamleta, yale yaliyokuwa yakitukia Mbinguni, kisha akashuka kwenye mlalo wa upinde wa mvua. Alifanya hayo yote katika muda wa kama dakika tano, katika kupumua kumoja, ilivyoonekana. Alipomaliza, aliruka juu hewani kama futi tatu, ilivyoonekana kwangu, vile, na kugonganisha visigino vyake pamoja. Akaja akijibana pale. Naye alikuwa na nafasi maradufu ya niliyo nayo. Akasema, "Hamna kabisa nafasi ya kutosha kwangu hapa kuhubiria," ndipo akaketi chini.

67 Nikawazia "Hicho ndicho ninachohitaji. Kama hicho kitamfanya mzee kujisikia namna hiyo, kingenifanyia mimi nini kama nitaipata chemchemi hiyo ya ujana?"

68 Mzee, mwenye umri wa miaka themanini na mitano, naye angeweza kufanya hivyo! Vema, jamani, alitoka akaja pale, kwa namna fulani alikuwa akishikilia. Lakini niliona hapo Roho huyo alipomgusa, aliufanya upya ujana wake kama tai, unajua.

69 Sasa katika kitabu cha Luka Mtakatifu ningependa kusoma kifungu kimoja kidogo tu ama viwili, kwa Maneno machache tu hapa, kuyaunganisha na jambo fulani ambalo limekwisha kusemwa, na yote kwa pamoja, na nyimbo ambazo zimeimbwa. Na Bwana aongeze baraka zake kwenye kusomwa kwa Luka Mtakatifu 19.

> *Naye Yesu alipoingia Yeriko alipita katikati yake.*
>
> *. . .tazama, palikuwa na mtu,* aliyeitwa *jina lake Zakayo, mkubwa mmoja katika watoza ushuru, naye ni tajiri.*
>
> *Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, asiweze kwa sababu ya umati wa watu, . . . ni mfupi wa kimo.*
>
> *Akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa kuwa atakuja kuipitia njia ile.*
>
> *Na Yesu, alipofika mahali pale, alitazama juu, akamwambia, Zakayo, shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako.*

70 Hapana shaka ulikuwa ni usiku wa usumbufu sana. Maskini jamaa huyo hakuwa amelala hata kidogo. Aligeukageuka na kugaagaa pande zote usiku kucha. Sote tunafahamu siku za

usiku wa namna hiyo: huwezi kutulia, huwezi kulala. Naye aligeukageuka usiku kucha, akigaagaa kila mahali.

71 Unajua, mke wake, Rebeka, alikuwa ni mwaminio, naye alikuwa amesukumwa kuhusika juu ya mumewe ambaye alikuwa na biashara huko Yeriko. Naye alikuwa ni mwanachama wa mashirika mengi ya siku hiyo, hapana shaka. Naye Rebeka alikuwa anamfahamu na—nabii jina lake Yesu wa Nazareti, ambaye walidai alikuwa ni Mwana wa Mungu. Naye alikuwa akitaka sana mumewe akutane na Mtu huyu.

72 Kwa sababu, yeye Rebeka alijua ya kwamba Wayahudi walikuwa wamefundishwa, ya kwamba, "Kama mtu alikuwa ni nabii, ya kwamba yale aliyosema yangetukia. Bali kama yale aliyosema hayakutukia, basi msimsikie." Mungu alikuwa amewaachia Neno, kwa manabii Wake. Hivyo ndivyo nabii alivyotambulikana.

73 Naye yule mtoa sheria mkuu, Musa, yeye pia alikuwa ameacha amri, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii mithili yangu. Itakuwa ya kwamba ye yote yule ambaye hatamsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali miongoni mwa watu."

74 Naye Rebeka alikuwa ameshawishika kabisa, wakati alipomwona Yesu wa Nazareti angeweza kusimama na kuwaambia watu mambo yaliyokuwa moyoni mwao, kutabiri mambo yatakayotukia, yakatimia vile vile hasa Yeye alivyosema, hayakushindwa hata wakati mmoja kutukia. Na Huyo alikuwa amesimama barabara katika Neno la Mungu. Rebeka aliamini jambo hilo.

75 Lakini Zakayo, mumewe, alikuwa amechangamana. Na, vema, ukweli wa mambo yenyewe ulikuwa kwamba, yeye hakuwa amewahi kumwona Yesu wakati wo wote.

76 Na kwa kweli hilo ni jambo baya, kujaribu kumpambanua mtu kabla hujamsikia. Hupaswi kufanya hivyo kamwe. Mara nyingi tungali tuna hatia ya jambo hilo, katika siku hii ya leo. Tunasikia juu ya mtu fulani, na, kabla hata hatujazungumza naye, sisi—sisi tungali . . . tayari tumetoa maoni yetu juu yake, kwa maoni ya mtu mwingine. Wala si jambo zuri. Tunapaswa kwenda, kujionea wenyewe.

77 Kama ilivyosemwa wakati mmoja, "Laweza neno jema lo lote kutoka Nazareti?"

78 Wakati Filipo alipokuwa amekwenda kumwona Nathanaeli na akamkuta chini ya mti, naye akasema, "Njoo, umwone Ambaye tumemwona, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

79 Akasema, "Sasa, laweza neno jema lo lote kutoka Nazareti?"

80 Alimpa moja ya maneno mazuri sana ambayo angaliweza kumpa. "Njoo, uone." Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo, ujionee mwenyewe.

81 Ndipo alipokuja, Yesu alimwona akija. Akasema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

82 Akasema, "Rabi," ambalo maana yake ni *mwalimu*, "ulipataje kunitambua?"

83 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

84 Hilo lilitosha. Kasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli," kwa maana aliona neno lile lile ambalo—ambalo Musa alikuwa amesema lingetukia. Hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, na huyu hapa mtu aliyekuwa amesimama barabara juu ya Neno.

85 Jinsi ambavyo maskini yule mwanamke pale kwenye kile kisima cha Samaria hapana budi alijisikia wakati alipotoka kwenda kuchota maji siku moja, na pale paliketi Mwanamume mmoja, Myahudi. Hapana budi alionekana mwenye umri wa miaka hamsini, ingawa Yeye alikuwa na thelathini tu. Hapana shaka kazi yake ilikuwa imemdhoofisha.

86 Walipokuwa na sikukuu ya—ya vibanda, wote walikuwa wakifurahi. Ndipo Yesu akapaza sauti kwa nguvu, kama ilivyonukuliwa muda mfupi uliopita, "Njoni Kwangu." Kwa hiyo basi akaanza kutoa mhadhara wake muhimu.

87 Na ninii—nao Wayahudi wakamwambia, "Unataka kusema umemwona Ibrahimu? Na Wewe ni mtu usiyepata umri wa miaka hamsini, unasema umemwona Ibrahimu? Sasa tunajua una wazimu." Na neno *wazimu* pale linamaanisha "kichaa." "Tunajua Wewe una kichaa. Una pepo."

88 Akasema, "Ibrahimu asijakuwapo, Mimi Niko." Huyo alikuwa ni yule MIMI NIKO aliyenena na Musa katika kijiti kilichowaka moto.

89 Nasi tunaona ya kwamba wakati alipokuwa ameketi... Alitaka kwenda apitie Samaria. Kwa sababu, Israeli ilikuwa imesikia ujumbe, Naye alikuwa akija sasa kwa zile jamii tatu: Wayahudi, Mataifa, na Wasamaria; watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Naye ananinii... Injili haina budi kuletwa kwao. Ndipo akaja kwenye mji ulioitwa Sikari, na hapo, akawa ameketi kisimani. Ndipo akawatuma wanafunzi Wake mjini, kununua chakula.

90 Maskini mwanamke mmoja akatokea. Tungemwita siku hizi, vema, pengine "alama ya hatari," jina fulani baya. Unajua ninachomaanisha. Na kwa hiyo akawa amemwona Yesu... Ninamaanisha, hakumwona Yesu hata kidogo ameketi kule, akiwa ni Mwanamume wa kawaida tu wa Kiyahudi ameketi ameegemea kwenye ukuta. Wa kile kisima kidogo, huko mwishoni mwa barabara, ya... mahali ambapo watu wa mjini walikuja kuchota maji yao. Maskini Jamaa huyu akiwa ameketi pale, hakuna anayemwona. Huyo mwanamke alikuwa amekuja

labda kama saa tano mchana, kuchota maji, maji ya familia ya siku hiyo. Ndipo akashusha ndoo kuyachota, na, kabla hajaweza kuyavuta, alimsikia Mtu fulani akisema, “Nipe maji ninywe.”

91 Akatazama pande zote na akaona kwamba ilikuwa ni Myahudi. Naye huenda akawa amesema kitu kama hiki, “Bwana, si kawaida kwa Wewe kusema jambo kama hilo. Mimi ni Msamaria. Wewe ni Myahudi. Wala sisi hatuna… Kuna ubaguzi hapa. Hatuna uhusiano kama huo mmoja kwa mwingine.”

92 Ndipo Yesu akaingia kwenye kuzungumza. Mazungumzo yakaendelea, kuhusu kama huyo mwanamke aliabudia Yerusalemu. Akasema, “Sisi Wayahudi tunajua tunachoabudu, kwa maana wokovu ni wa Wayahudi.” Na mazungumzo yakaendelea kwa kitambo kidogo. Na baada ya kitambo kidogo Yeye akamwambia, “Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

93 Kasema, “Umesema kweli, kwa maana umekuwa na waume watano, naye unayeishi naye sasa siye mumeo.”

94 Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe u nabii.” Sasa, unaona, hawakuwa wamepata nabii kwa muda wa miaka mia nne, tangu Malaki. Kasema, “Naona ya kuwa Wewe u nabii. Tunajua, Masihi atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya. Hiyo ingekuwa ni ishara ya nabii. Masihi ajapo, atatwambia mambo haya.”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

95 Akakimbia kwenda mjini na kusema, “Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo yote niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Jinsi ambavyo Nuru hiyo ilivyotokea kwanza juu ya maskini mwanamke aliyekuwa katika hali hiyo!

96 Ni ninii—lilikuwa ni kemeo la jinsi gani kwa hao makuhani wa hekaluni wa siku hiyo, waliomwona Yeye akifanya jambo lilo hilo, na kumwita Yeye, “Beelzebuli, ibilisi, roho mchafu akifanya kazi hizi”! Wakati, Maandiko yakidhihirisha waziwazi sana ya kwamba ingekuwa ni Masihi. Sasa sisi…

97 Rebeka alikuwa ameona haya yote, naye alikuwa anatamani sana kwamba mumewe angeweza siku moja kuketi mahali ambapo Yesu wa Nazareti alikuwa. Naye alifahamu kwamba Yesu alipaswa kuwa huko Yeriko, mji wake Rebeka, siku hiyo. Naye akaingia kwenye kumwombea. Ninatumaini kuna akina Rebeka wengi hapa usiku wa leo, kwamba utamwombea mumeo, kwamba siku moja Yesu atapita kwenye njia waliko. Naye alikuwa ameomba usiku kucha, kama vile tungelifanya jambo hilo kama drama.

98 Nanyi mnajua, wakati mtu anapoanza kukuombea, kwa uaminifu, hu—hupati raha. Unaweza kujua, kuna kitu fulani kinachotendeka.

99 Ndipo basi karibu na asubuhi, tungesema. . .Zakayo alikuwa na tabia ya kuamka kidogo amechelewa, kwa sababu, labda tutasema, alikuwa na hoteli, na aliacha ninii. . .uongozi wa—wake, na kadhalika, waendeleze biashara hiyo. Bali asubuhi hiyo, aliamka mapema sana, akajiweka nadhifu sana, na akavaa nguo zake zilizo nzuri sana. Basi Rebeka, baada ya kuomba usiku kucha, na kuona ya kwamba Zakayo hatulii hata kidogo. . .

100 Na sikiliza, ewe Rebeka, unapomwona Zakayo wako kwa namna fulani akiingiwa na wasiwasi, kumbuka tu, Mungu anayajibu maombi, unaona. Hivyo ndivyo inavyokuwa. Unapomwona akifikia mahali ambapo hawezi kuzungumza na wewe maneno mazuri, kumbuka tu, endelea kushikilia. Si muda mrefu hata Mungu atakapompitia kwenye njia hiyo.

101 Aliingiwa na wasiwasi sana. Alipoamka, alivaa mavazi yake yaliyo mazuri sana. Na ninaweza kumwona Rebeka akigeuka na kusema, "Zakayo, umeamka mapema sana asubuhi ya leo, mpenzi wangu."

102 "Loo, ndiyo. Ha, ninaninii tu, ha, ha-ha-ha, mm. Unajua, Nili—Nilifikiri tu ningetoka nje kupunga hewa kidogo."

103 Lakini, alikuwa amewazia, "Nisingeweza kumwondoa Jamaa huyo mawazoni mwangu. Unajua nitakalofanya? Nitashuka niende kule chini langoni ambako anaingilia. Na wakati atakapoingia kwenye lango lile, nitampa ukweli Wake, kwa kumfanya mke wangu atoke huko nje, kwenye mikutano hii, na kupiga makelele namna hii. Nitamwambia ninayomwazia." Unajua, kwa kawaida watu wanajiumbia kinyongo cha namna hiyo, unajua, wanaposikia tu jambo fulani.

104 Kwa hiyo akajitengeneza vizuri sana. Akachopoka kisiri. Akaangalia huko nyuma, nyumbani, na aone kama kuna mtu anayeangalia, na ilionekana kana kwamba hakuna mtu aliyekuwa akiangalia. Lakini Rebeka alikuwa akiangalia kupitia kwenye mwanya wa dirisha, akiona yale aliyofanya. Na badala ya kuelekea kwenye hoteli yake, alishuka kuelekea kwenye Barabara Nyofu.

105 Unajua, kwa kawaida unampata Yesu kwenye Barabara Nyofu. Hiyo ni kweli. Mnyofu katika biashara yako! Ukitaka kumwona, uwe mwaminifu, uwe mkweli, uwe mnyofu kwa Mungu na wanadamu, uwe mnyofu kwa jirani yako.

106 Kwa hiyo akachopokea kisiri barabarani, maana alijua Yeye ataingilia kwenye lango hili fulani. Alikuwa amecheleweshwa kidogo asubuhi hiyo, kwa sababu vipofu wawili walitaka kuponywa, kama Maandiko yanavyotwambia, Naye alikuwa amewaponya hao. Ndipo alipofika kwenye lango ambapo Yesu alipaswa kuingilia. . .Unajua, Biblia ilisema, "Alikuwa kwa namna fulani mfupi wa kimo." Ndipo alipofika pale, baadhi ya wale watu mashuhuri sana walikuwa wamesimama pale, wala

hata asingeweza kupata nafasi, ya kwenda kumwona. Walikuwa wanangojea kwenye kuta na kila mahali.

107 Unajua, kuna jambo fulani kuhusu kitu hicho, kwamba, Yesu anapokuja karibu, daima inavutia usikivu kwa namna fulani. Walikuwa wako pale, wakiwa tayari kuimba, "Hosana!" Nao . . .

108 Akasema, "Sasa, kamwe sitaonekana hapa. Wala sitaweza kumwona Yeye, maana Yeye labda atatembea katikati ya barabara, akiwa na mlinzi binafsi, wala sitaweza kumwona Jamaa huyu. Lakini mimi siamini ya kwamba Yeye ni nabii, kwa maana nimefundishwa ya kwamba siku za unabii na siku za miujiza zimepita." Unajua, wakati haujabadilika sana tangu wakati huo.

109 Kama Mungu alipata kuwa Mungu, Yeye yungali ni Mungu. Kama siye, basi Yeye kamwe hajapata kuwa Mungu. Huwezi kabisa kusema Yeye ni Mungu wakati mmoja, wala si Mungu wakati huo mwingine. Yeye hazeeki. Hawezi kubadilisha nia Yake. Hana budi kusimama na maamuzi Yake. Kwa hiyo, unaweza kujua yakini kwamba, yale Yeye aliyosema, hayo atayafanya. Hivyo ndivyo . . .

110 "Ibrahimu alimwamini Mungu, akaviita vitu ambavyo vilikuwa kinyume kana kwamba vilikuwa—havikuwako. Mambo yaliyoonekana ni halisi, yale ambayo macho yake yangeweza kuona, bali yalikuwa ni kinyume cha Neno la Mungu, naye—naye kwa ajili ya . . . haninii . . . hata hakuyaangalia. Aliyaita kana kwamba hayakuwako. Alimwamini Mungu." Hakushikilia tu kwa siku moja. Aliendelea moja kwa moja katika maisha, miaka ishirini na mitano, kabla Isaka hajapata kuzaliwa. Naye akazidi kupata nguvu, wakati wote.

111 Sisi leo tunadai kuwa, kwa neema, na kwa rehema na kwa kufanywa wana wenye mamlaka na Kristo, kwamba tunakuwa Uzao wa Ibrahimu, wala hatuwezi kumtumaini Mungu saa ishirini na nne. Lakini Uzao halisi wa Ibrahimu hulishika Neno la Mungu wala hakuna kitu kitakachomwondoa kwake.

112 Mungu alimwambia Ibrahimu, wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye Sara akiwa na sitini na mitano, wao watampata mtoto. Mbona, waliondoka na wakanunua pini zote na vijiatu, na kujiweka tayari kwa ajili yake. Hiyo ni kweli. Hakukuwako na jambo la kuwazuia. Walijua jambo hilo.

113 Siku ishirini na nane za kwanza zilipita. Akasema, "Unajisikiaje, Sara?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu! Tutampata, hata hivyo."

"Unajuaje?"

"Mungu alisema hivyo. Hilo latosha."

Mwezi uliofuata, "Unajisikiaje?"

"Hakuna tofauti."

114 "Vema, ni muujiza mkubwa zaidi kuliko hapo nyuma sasa. Umechelewa kwa miezi miwili." Unaona?

Miaka ishirini na mitano, "Unajisikiaje, Sara?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu! Tutampata, hata hivyo. Mungu alisema hivyo."

115 Na halafu tunajiita Uzao wa Ibrahimu. Yale Mungu asemayo, Mungu anaweza kuyafanya, kufanya yale aliyosema angefanya. Mimi siwezi kudumisha neno langu sikuzote. Wala wewe huwezi. Bali Yeye hana budi kulitimiza, ili awe Mungu.

116 Kwa hiyo, tunaona ya kwamba mtu huyu hakuamini jambo hilo, maskini mfanyabiashara huyu wa mji wa Yeriko. Alikuwa na biashara kubwa. Alidhani mambo yalikuwa sawasawa. Alikuwa amependwa na makuhani na sinagogi. Alikuwa anapendwa na makanisa, na Makiwani, na—na mengi ya mashirika ya siku hiyo, kama ambavyo tungesema. Hata hivyo, hilo halimaanishi ni Mungu, bado.

117 Kustawi hakumaanishi ni Mungu kamwe, daima. Wakati mwingine ni kinyume chake.

118 Mungu alisema, "Mlipokuwa mmekaa kondeni," aliwaambia Israeli, katika damu yake mwenyewe, wakati huo walikuwa tayari kumtumikia. Bali walipojitosheleza, alifikiri amejitosheleza, basi hakutaka kuwa na ushusiano wo wote Naye tena, akampa kisogo.

119 Isaya alipata mfano huo kutoka kwa yule mfalme Uzia, maana Uzia alikuwa mtu mkuu mradi tu alijinyenyekeza mbele za Mungu. Hakushiriki katika siasa. Alishikamana na Mungu, na Mungu akambariki. Ufalme wake ulikuwa unakaribia ule wa Sulemani. Ila, wakati alipoingiwa na majisifu!

120 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Kamwe msiruhusu jambo hilo lilipate shirika hili la wafanyabiashara, la sivyo mtaangamia kama hao wengine. Kila wakati watu wanapofikia mahali mpaka—mpaka ustawi unaanza kuyapofusha macho yao yasilione Neno la Mungu, wanaharibikiwa.

121 Uzia alikuwa ni mtu mashuhuri, bali alijaribu kupachukua mahali pa mhubiri, siku moja, kuingia na kufukiza ubani. Ndipo kuhani mkuu, akiwa pamoja na wingi wa makuhani wengine, akaja na kumwambia, "Hupaswi kufanya jambo hilo. Wewe ni mlei."

122 Na ninyi wafanyabiashara kumbukeni jambo hilo, pia. Sisi wahubiri tuna wakati mgumu wa kutosha kukiweka Kitu hiki sawa. Si kazi ya walei. Walei wana sehemu yao, bali mimbara ni ya mhudumu ambaye amewekwa wakfu. "Mungu anaweka, Kanisani, watu kwa ajili ya mambo haya."

123 Na halafu basi tunaona kwamba alichukua chetezo na kuingia, hata iweje. Ndipo Mungu akampiga kwa ukoma, naye akafa mwenye ukoma. Unaona, tunapojikuza!

124 Zakayo alikuwa karibu katika hali hiyo. Alikuwa amestawi. Alikuwa na uhusiano mwema na rabi. Alikuwa na uhusiano mwema na mashirika yote. Kwa hiyo akawazia, kama akipatwa na shida, angesaidiwa, Baraza la Wazee lilikuwa linamuunga mkono. Anasimama langoni. Ataenda kufanya jambo fulani sasa. Atatoka aende na kumshika Jamaa huyu, na kumwambia uso kwa uso, "Wewe ni nabii wa uongo. Huna lo lote. Unachukua tu telepathia ya akili, na kuwadanganya watu." Unaona, yeye hakusimama asome Neno.

Hapo ndipo kosa linapofanyika leo.

125 Kama Israeli wangalifanya hivyo badala ya kufanya waliyofanya, wangalikuwa na hali bora zaidi leo. Bali ilibidi wafanywe hivyo. Ilibidi litimizwe, kusudi macho yao yapofushwe, ili sisi tupate kuwa na nafasi. Isingalikuwa hivyo, tungekuwa wapi sisi? Angalia.

126 Lakini alipofika kule, anakuta kwamba hata hawezi kuona kitu. Hawezi kuiona barabara, kuna watu wengi sana waliokusanyika, kila mahali. Kwa hiyo anawazia, "Unajua nini? Yeye anapanda . . . Wananiambia, Rebeka aliniambia, ya kwamba, leo, alikuwa yuaenda kula huko—huko Lavinski." Natumaini hakuna Lavinski hapa. Bali, hoteli yake, mshindani wake. En-he. Kwa hiyo alikuwa akienda kula kwenye hoteli yake, labda. "Kwa hiyo ninajua, jinsi ya kufika pale, itatubidi kushuka chini, tupige kona kwenye Barabara Nyofu hapa, tutelemke kwenye Barabara Kuu ya Haleluya," ndivyo tutakavyoiita.

127 Hayo ni majina yasiyo na ladha, bali ninafanya tu jambo hilo nipate kufanya tamthiliya yangu. "Nasi hatuna budi kupiga kona hapa, kutoka kwenye Barabara Nyofu, kuingia kwenye Barabara Kuu ya Haleluya." Hebu kaa tu kwenye barabara hiyo muda mrefu vya kutosha, utaingia kwenye Barabara Kuu ya Haleluya. Utadumu kuwa mnyofu.

128 Kwa hiyo anashuka anaenda, upesi. Akasema, "Mimi ni mfupi wa kimo." Akakiweka nadhifu hicho kimo chake kifupi: akachana ndevu zake kwa chini; akahakikisha amejinyunyizia manukato vizuri; kucha zake zimesuguliwa vizuri. Akasimama pembeni, akasema, "Nitamwona atakapopitia hapa, nami nitamwambia yale ninayomwazia atakapopitia hapa." Kwa hiyo anasimama pembeni.

129 Ndipo akaanza kuwazia, "Unajua nini? Kundi lile lile litamfuata. Watafika papa hapa, na wataninii tu . . . Mimi ni mfupi sana, kamwe sitaweza kumwona, kwa hiyo haitafaa kitu kusimama hapa. Sitakuwa na nafuu zaidi hapa ya vile nilivyokuwa nayo sehemu ile niliyokuwa. Na, unajua, unaamini

kile—kile nitakachofanya? Huu hapa mti wa mkuyu umekulia hapa, kwa hiyo ninafikiri nitapanda tu juu ya mkuyu huu. Na ndipo nitaweza kumwona, na kumwangalia vizuri atakapopitia hapa. Kwa hiyo hataweza kuniona kamwe huko juu kwenye ule mti. Na kuna tawi linalojitokeza pale; nami nitaketi moja kwa moja juu ya lile tawi na kumwangalia atakapotokea, na atakapoondoka. Nitamtazama vizuri sana Jamaa huyu."

130 Na kwa hiyo, muda si muda unajua, alianza kujaribu kuona jinsi tawi la kwanza lilivyokuwa juu, na kidogo lilikuwa mbali kulifikia.

131 Unajua, kwa kweli, hatua ya kwanza kidogo iko mbali na uwezo wetu. Inatubidi kuikubali kwa imani. Naam. Kidogo ni zaidi ya vile akili ya mwanadamu inavyoweza kuielezea. Huwezi kumwelezea Mungu. Kama ukiweza, basi hakubaliki tena kwa imani. Inakubidi kumwamini. "Mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii."

132 Kwa hiyo tunamwona jamaa huyu mfupi anayejulikana sana, mmoja wa wafanyabiashara wa mji huo, akasema, "Sasa, nitaupandaje?" Na labda huenda ikawa wanaokusanya takataka hawakuwa wamepitia hapo asubuhi hiyo, na kulikuwa na mapipa yamekaa pale pembeni, yamejaa ta—takataka za mji. Kwa hiyo wao. . . Yeye akasema, "Kama ningeweza kuchukua pipa lile, ningeweza kulifikia na kulishika lile tawi."

133 Ni ajabu, jinsi ambavyo Mungu huwafanya watu wafanye mambo ya kuchekesha. Kwa hiyo, lakini, unajua, kama umekusudia unataka kumwona Yesu, utafanya mambo ya aibu, kama umekusudia unataka kumwona; wewe u—wewe kweli ni mwaminifu, unataka kweli kujua hayo yote ni Kitu gani.

134 Na hayo yalikuwa ndiyo maoni ya Zakayo. Alitaka kujua hayo yote yanahusu kitu gani, aliyokuwa akisikia. Kwa hiyo anasema, "Sasa hakuna mtu hapa karibu, kwa hiyo nitachopoka na kushika lile pipa la takataka na kulivuta hapa, na kulileta hapa kwenye m—mti. Na ndipo ninaweza kufika juu kwenye tawi la kwanza, na kufika juu—juu ya barabara wakati atakapopitia hapa." Lakini wakati alipoanza kuvuta lile pipa, lilikuwa ni zito sana kwake kulivuta. Alikuwa kwa namna fulani ni mtu mfupi, mwenye umbo dogo. Jambo pekee la kufanya, basi, itamlazimu kulibeba. Sasa, alikuwa amevaa nguo zake nzuri.

135 Unaona vile Ibilisi anavyofanya? Anajaribu tu kuweka kila kitu njiani mwako. Kwa hiyo yeye—atasogeza kila kitu, kila tashwishi, kila hitilafu anayoweza, kukuzuia usione yaliyo Kweli. Yeye ni hodari sana tu wa kufanya jambo hilo.

136 "Kwa hiyo nimevaa nguo zangu zilizo nzuri sana," huenda ikawa alisema hivyo. "Na hapa, mimi—mimi, kama nikishika pipa hilo la takataka, nitachafuka."

137 Unajua, kuna baadhi ya watu wanaofikiri, kuketi kwenye mkutano kama huu kunaweza kukutia uchafu kidogo, kwa namna fulani miongoni mwa shirika na watu mashuhuri wa mjini. Lakini kama kweli umekusudia kumwona Yesu, utakuja, kwa vyo vyote. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, kuna jambo moja tu la kufanya, kama mtu amekusudia kumwona Kristo, hakuna kitu kitakachomzuia.

138 Kwa hiyo ananyosha mkono na kulishika pipa hili la takataka, naye huyu hapa anakuja. Mara tu alipolikumbatia mikononi mwake, vizuri, washindani wake walitokea pembeni, wawili ama watatu wao. Wakasema, "Vema, mwangalieni Zakayo. Amebadilisha kazi yake. Anafanya kazi ya mji sasa." Ningewazia maskini uso wake ulikuwa mwekundu sana.

139 Sijui, usiku wa leo, kama bosi angaliingia humu na kuwaona baadhi yenu ninyi wafanyabiashara hapa, mmeketi kwenye mkutano kama huu unaoitwa "watakatifu wanaojifingirisha," sijui kama uso wako . . . Vema, tayari umetambulishwa, kwa hiyo afadhali utulie sasa. Zakayo tayari alikuwa amelishika mikononi mwake; alikuwa tayari amejitangaza. Na wewe tayari umekwisha kufika hapa, kwa hiyo afadhali uketi kimya, endelea uyapitie haya, ukiwa umeketi hapo ndani.

140 Alikuwa ameikumbatia hiyo ndoo ya takataka. Ni jambo la jinsi gani kwa mfanyabiashara! Huyu hapa anakuja, uso wake ukiwa mwekundu. Nao wakisema, "Vema, unajua nini, Zakayo?" Unajua, hali imekuwa mbaya sana, biashara imekuwa ngumu, kwa hiyo anatafuta namna. Wanasema, "Huyu hapa. Sasa ameajiriwa na mji. Ninajua, ninajua biashara yake imekuwa mbaya, angalia aina ya kazi aliyo nayo."

141 Alikuwa amekusudia kumwona Yesu, haidhuru. Alikuwa amesikia habari hiyo, naye alitaka kujua yeye mwenyewe.

142 Mungu laiti kila mtu angalichukua msimamo huo. Kama ulipata kusikia habari Zake, tafuta kujua. Yeye hajafa. Yeye yu hai, ni mkuu tu mahali hapa usiku wa leo kama alivyokuwa kwenye pwani za Galilaya. "Tazama, Mimi niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Kama hivyo sivyo, basi Yeye alikuwa ni Masihi wa uongo; Yeye hakuwa yule—yule Masihi anayepaswa kuwa. Lakini kama kweli anadumisha na kutimiza ahadi Yake, Yeye angali ni Mungu anayejidhihirisha kwa watu. Ingembidi kufanya mambo yale yale aliyofanya. Hiyo ndiyo njia Yake ya kufanya mambo. Ingembidi kujionyesha Mwenyewe jinsi alivyofanya wakati huo. Waebrania 13:8, Paulo akiwaambia Wayahudi, yeye alisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo, Yeye hana budi kuwa ni yeye yule katika tabia, yeye yule katika nguvu, yeye yule katika kila kitu alichokuwa. Hana budi kuwa ni yeye yule leo.

143 Mara kwa mara, tunaona kazi za Mungu, ninajua kuna unafiki uliochanganywa nazo. Unapoona dola ya bandia, hiyo inawaambia nini, ninyi wafanyabiashara? Utaacha kazi? Utatoa pesa zako zote katika benki na kuzitupa m—mtoni kwa sababu ulikuta dola ya bandia? Hiyo dola ya bandia inamaanisha tu ya kwamba kuna dola halisi iliyotengenezwa kutokana na hiyo. Na Pentekoste imejaa uigaji wa kimwili. Lakini hilo lina maana gani? Kuna iliyo halisi pale mahali fulani. Ni mtu fulani akijaribu kuiga jambo fulani ambalo mtu mwingine analo halisi kabisa. Ni risiti tu ya kujipatia riziki. Ni kitu tu kiliigwa kutokana na Kitu halisi, kilicho nyuma ya kitu hicho, ambacho mtu fulani anajaribu kuiga.

144 Kwa hiyo tunaona, Zakayo anachukua ndoo yake ya takataka. Na washindani wake wanashuka wakitembea barabarani, wakimcheka. Lakini haikuleta tofauti yo yote. Alikuwa amekusudia kumwona Yesu. Ndipo angekuwa na maoni juu Yake.

145 Tungeweza tu kupata hali za namna hiyo miongoni mwetu, kama tu tungeweza kuazimia, ya kwamba tutatafuta kujua kwamba Haya yote yana maana gani, kama ni ile Kweli. “Mungu akiwa ndiye Mungu, mtumikieni.” Nabii Eliya alisema jambo hilo, juu ya Mlima Kameli. “Mungu akiwa ndiye Mungu, mtumikieni. Kama yeye Baali ni Mungu, mtumikieni.” Kama Yesu Kristo hawezi kujitangaza Mwenyewe kama vile vile tu alivyokuwa daima, basi Yeye hakufufuka kutoka kwa wafu.

146 Kama tunakazana tu kuwaingiza watu ndani kwa ushawishi wa kisaikolojia, kama tunaweza tu kuwabadilisha kutoka Methodisti wawe Baptisti, ama Baptisti wawe Wapentekoste, ni kitu gani? Ni kundi la saikolojia. Hiyo ni kweli.

147 Mungu aliye hai Ambaye aliziumba mbingu na nchi angali ni Muumba yeye yule. Yeye angali, kwa tabia, Mungu yeye yule aliyewahi kuwa. Nina furaha nilimwona Mungu kabla kanisa halijanipata, kujua ya kwamba Huyo alikuwako.

148 Ninaona ugomvi wao, na mizozo, na malalamiko. Daima imekuwa hivyo, kote. Walikuwa na jambo lile lile, kote katika Maandiko.

149 Lakini jamaa huyu mdogo alitaka kumwona Yesu, naye alikusudia kufanya hivyo. Alikuwa ni mfanyabiashara, naye alitaka kufanya biashara vizuri. Kwa hiyo, yeye, alipokusudia . . . Mkewe akiwa nyumbani, akiomba, na maombi ya Rebeka yalikuwa yakimfuata. Ndipo jamaa huyo mdogo ilibidi apande juu ya mti. Ilimbidi kukwea juu ya ninii . . .

150 Sikumaanisha jambo hilo. Huo ni msamiati wa Kusini, wa “kukwea.” Ni wangapi wanaojua maana ya “kukwea juu ya mti”? Vema, ni wangapi wenu Wakentake mlio hapa hata hivyo?

151 Ilimbidi kuukwea huo mti, kuupanda huo mti. Naye huyu hapa, ameketi pale sasa juu ya mti, akipangusa takataka kutoka

kwenye vazi lake jipya; akitoa vibanzi vidogo kutoka kwenye magoti yake na mikono, hapo ambapo alikuwa amepanda huo mti. Lakini haidhuru ni jambo gani lililotukia, yeye alikusudia kumwona Yesu. Na kama wewe kweli . . .

152 Nisikilizeni. Kama kweli umekusudia kumwona Yeye, hujali yale yatakayokubidi kupitia, ni ukosoaji wa kiasi gani, yale watu wengine wanayosema. Ukitaka kumwona Yesu, utafanya jambo lo lote upate kumwona Yeye. Utangojea zamu yako. Utafanya lo lote unalopaswa kufanya, upate tu kumwona Yeye.

153 Shida yake ni kwamba, ya siku hizi, hawaoni kiu vya kutosha. Watu hawana kiu na njaa ya kutosha. Ninaamini Kanisa linapaswa kuwa limekolea chumvi zaidi ya vile lilivyo.

154 Chumvi husababisha kiu. Chumvi ndiyo ladha kama ikigusana. "Lakini kama chumvi imepoteza ladha yake, haifai kitu tena," bali inakuwa ni madhehebu. Hiyo ni kweli. Lakini inakubidi kuwa na ladha ya jambo hilo. Ladha hiyo ni chumvi, hiyo nguvu.

155 Kama mtu akimwona Kristo akiishi ndani yako, itamfanya awe na kiu apate kuwa kama wewe. Itamfanya amwone Yesu ndani yako, itamfanya amwone Mungu.

156 Walijuaje ya kwamba Musa alikuwa ni wa Mungu? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Nao walijua ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye.

157 Sasa tunaona, kama vile Petro alivyosema kwenye ile Siku ya Pentekoste, juu ya, "Enyi wanaume wa Israeli, jinsi mlivyo- . . . " Akakishtaki kizazi hicho kwa ajili ya kumsulibisha Mwana wa Mungu. Kasema, "Enyi . . . Yesu wa Nazareti, Mtu aliyedhihirishwa na Mungu miongoni mwenu, akathibitishwa na Mungu, kwa ishara na maajabu ambayo Mungu aliyafanya kupitia Kwake; mmemchukua Mfalme wa Uzima, kwa mikono ya watu wabaya, na kumsulibisha."

158 Je! Nikodemo hakuelezea hisia zao zote vizuri? Ilikuwa ni fahari ya kijamii kuwa mfuasi wa kitu fulani, jambo ambalo liliwazuia wasimwone Yesu. Akamwambia, "Rabi, tunajua ya kwamba Wewe ni Mwalimu, anayetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu angeweza kufanya ishara hizi isipokuwa Mungu yu pamoja naye." Walitambua jambo hilo. Lakini kwa sababu ya fahari ya kijamii, waliona aibu kukubali jambo hilo.

159 Walipaswa kuwa kama yule kipofu ambaye Yesu alimponya.

Walisema, "Mtu huyu ni mwenye dhambi."

160 Yeye akasema, "Ni jambo la kushangaza. Ninyi, viongozi wa siku hii, wala hamjui Mtu huyu alikotoka?" Kasema, "Kama Yeye ni mwenye dhambi ama si mwenye dhambi, sijui mimi. Lakini jambo hili moja ninajua: ambapo wakati mmoja nilikuwa kipofu, sasa naweza kuona." Jambo ndilo hilo. Hilo ndilo jambo moja alilolijua.

161 Ninapenda ushuhuda halisi wa watu wanaosimama katikati ya watu na kusema, “Ninajua kuna jambo fulani. Jambo fulani lilinitukia.”

162 Kama vile nilivyojaribu kusema habari za yule dada mweusi, “Mimi siko vile ninavyotaka kuwa, au siko vile ninavyopaswa kuwa, bali hata hivyo ninajua siko vile nilivyokuwa.” Kitu fulani kilikuwa kimemshika.

163 Zakayo, akiketi pale, jinsi alivyokuwa amechafuka, akiketi pale. Nanyi mnajua . . .

164 Nisikilizeni. Watu wanaomwamini Mungu, wanapatwa na machafuko, hata hivyo. Wanafanya mambo ambayo ni kinyume kabisa na mwenendo wa siku zao.

165 Sikilizeni habari za Musa. Siku moja, akiwa mchunga kondoo. Shujaa mkuu huko Misri, kuwakomboa watu wake, naye alikuwa ameshindwa. Ndipo akawa mchunga kondoo, kwa muda wa miaka arobaini. Mzee mzuri, ametulia, jamaa mzuri, alikuwa na mke na mtoto; Sipora, Gershomu. Sasa tunaona ya kwamba, baada ya Mungu kumpata, naye akamwona Mungu katika kijiti kilichowaka moto, kesho yake alimweka mkewe juu ya nyumbu, mtoto nyongani mwa mama. Ndevu nyeupe zikipeperuka. Fimbo iliyopinda mkononi mwake, akimwongoza nyumbu huyu; upepo ukivuma. Kichwa chake chenye upara kiking’ara, katika jua kali, akishuka kwenda Misri.

Mtu fulani angesema, “Musa, unafanya nini?”

166 “Ninashuka kwenda Misri, kuiteka.” Uvamizi wa mtu mmoja, bali aliiteka. Kwa nini? Mungu alimwambia afanye hivyo. Hiyo ndiyo sababu yake. Unaona, lilionekana—lilionekana kuwa ni la kiwenda wazimu. Ambapo, mtu huyo alikuwa ametoroka toka mahali hapo, sasa anarudi moja kwa moja.

167 Hivyo ndivyo watu wanaompata Mungu, wanavyoazimia kumwona Yeye.

168 Huyu hapa ameketi. Baada ya kitambo kidogo, akaanza kuwazia, “Unajua, Rebeka aliniambia Mtu huyu alikuwa ni Nabii. Ninashuku hilo sana. Siamini katika jambo hilo. Siamini ya kwamba kuna manabii wa siku hizi. Kama wangalikuwako, kuhani wangu angaliniambia habari zake. Kuhani wangu ni mmoja wa watumishi wa Mungu, kwa hiyo angaliniambia habari zake.” Hilo ni sawa.

169 Lakini, unaona, kamwe dini ya kimadhehebu ya ulimwengu haijawahi kumkumbali mjumbe kutoka kwa Mungu wakati wo wote, kamwe haijawahi. Hivi Yesu hakuwaambia, “Enyi Mafarisayo vipofu, mnapaka rangi makaburi ya manabii, nanyi ndio mliowaweka mle ndani. Ni nani kati ya manabii waliotumwa na Baba, ambaye hamkumwua na kumweka

kaburini, kwa maana alionyesha kuja kwa Yule Mwenye Haki?" Unaona?

170 Hapo, basi, tunaona, huyu hapa, ameketi pale juu. Unajua nini? Natumaini drama hii haisikiki ya mzaha, bali nitawazia yeye alisema, "Sasa, ngoja kidogo, kama ikitokea kwamba Jamaa huyu ataniona nimeketi hapa kwenye tawi hili!" Naye akaketi mahali ambapo matawi mawili yalikingamana. Naye alikuwa ameketi pale, akiwazia jambo hilo.

171 Hapo ni mahali pazuri pa kuketi, mahali ambapo njia zako na njia za Mungu zinapokutana. Hapo ni mahali pazuri pa kuwazia mambo. Nami ninatumaini ya kwamba kila mtu ndani hapa, ambaye hajapata kukutana Naye, na kwa kweli unajua ya kwamba umezaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu, ya kwamba umeketi kwenye tawi hilo usiku wa leo. Lakini, ninyi wafanyabiashara, ninatumaini ya kwamba mmeketi mahali ambapo tunajaribu kusema Zakayo aliketi, juu ya mkuyu, wenye matawi ambapo njia mbili zilikutana, yako na ya Mungu.

172 Ndipo akasema, "Unajua yale ninayofikiria nitafanya? Nitavuta tu majani haya hapa na kujificha." Akajifunika kabisa. Akajiachia dirisha moja dogo apate kuchungulia, unajua, jani moja, angeweza kulivuta chini, na kusema, "Nitamwona atakapokuja, bali kamwe hataniona. Hatajua kamwe niko hapa juu."

173 Kwa hiyo wakati alipokuwa ameketi pale, punde si punde, akiwazia juu yake, kulikuja kelele hapo kwenye kona.

174 Ni jambo la kushangaza, bali, kila mahali Mungu alipo, panaonekana kuwa pana kelele nyingi. Hilo ni la ajabu, bali ni kweli.

175 Unajua, Isaya, hekaluni, baada ya kifo cha Uzia, alikuwa huko chini. Naye akasikia kelele, na hekalu lote lilikuwa likitikisika. Nguzo ziliondoka mahali pake. Na kulikuwako na Malaika, Maserafi, pale, ambao ni Makerubi, wateketezaji wa dhabihu, kumpa mwenye kutubu haki ya kwenda madhabahuni. Hao Wenye Uhai wakuu, walio zaidi ya Malaika, wakiwa wamefunika nyuso Zao kwa mbawa Zao, na mbawa zimefunika miguu Yao, na wakiruka kwa mabawa mawili, wakisema kwa sauti kuu, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi."

176 Kama Malaika hufunika uso wake mtakatifu, kwa kukutana na Mungu, tutachukuaje kanuni ya imani na kujifunika zetu na hiyo? Itahitajika Damu ya Yesu Kristo kutufunika, ndipo tunakuwa ni wana. Si mtindo wa *hiki*, au mtindo wa *kile*, bali ile Damu. Mungu daima ameninii . . . Mahali pake pekee pa kukutana na mwanadamu kwa ajili ya ushirika ni chini ya Damu iliyomwagika, ambapo mbegu ya Uzima . . .

177 Katika ile dhabihu ya kale chini ya—ya torati ya Musa, walileta mnyama. Na wakati walipoipasua hiyo seli ya damu

ya mnyama huyu, mwana-kondoo, mwabuduo aliabudu. Lakini uhai uliokuwamo katika mnyama huyo usingemrudia huyo mwabuduo, kwa maana ulikuwa ni uhai wa mnyama bila ya nafsi. Wala usingeweza kumrudia mwabuduo. Kwa hiyo ilikuwa tu ni ku—kuificha. Palikuwa ni mahali tu pa kudumu mpaka wakati fulani.

178 Lakini basi wakati vena ya Imanueli ilipopasuliwa, Yesu hakuwa Myahudi wala Mmataifa. Unaona? Jinsia ya mwanamume hutoa mbegu kupitia katika himoglobini, na seli ya damu inatoka kwa mwanamume. Mwanamke . . .

179 Na ninyi Wakatoliki, si kwamba nataka kutofautiana nanyi, bali mnamwita yeye, "Mariamu, mama wa Mungu," Mungu angewezaje kuwa na mama? Yeye alikuwa ni kiangulio.

Mnasema, "Vema, ya—yai lilitoka kwa mwanamke."

180 Lakini lile yai halikutoka kwa Mariamu. Kama lile yai lilitoka kwa Mariamu, basi ilibidi kuwepo na mhemko. Angalia mahali unapomweka Mungu. Mungu aliumba vyote viwili yai na seli ya damu pia.

181 Alikuwa si Myahudi wala Mmataifa. Alikuwa ni Mungu, si pungufu kwa cho chote. Alikuwa ni Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili. Hivi Yeye hakusema, tunasoma katika Maandiko, ya kwamba, "Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake"? Yeye alikuwa ni Imanueli. Alisema, "Kwangu Mimi, ambaye . . . "

182 Yeye alisema katika Maandiko hapa, hasa, "Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? Ni wapi nimeshindwa kufanya yale hasa yaliyoandikwa juu Yangu? Yachunguzeni Maandiko. Mnadhani mna Uzima wa Milele, katika kuyachunguza, Na hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Bali kama ninazifanya kazi hizo, ingawa hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi ninazofanya, kwa maana zinashuhudia kwamba Mimi ni Nani."

183 Loo, jinsi Mkristo alivyopungukiwa sana leo, na majaliwa ambayo Mungu amempa, na juu ya mambo yaliyo katika Biblia! Jinsi ambavyo ningetaka kuchukua somo kutoka hapo! Wakati hautaruhusu jambo hilo.

184 Alisikia sauti hiyo. Akasimama. Akasema, "Vema, hao hawana budi kuwa ni wale watakatifu wanaojifingirisha wanaokuja." Akashusha lile jani chini, akangoja kidogo. Baada ya kitambo kidogo, aliona, wakijitokeza kwenye kona wakija.

185 Hapana budi kulikuwako na jamaa mmoja mkubwa, mwenye nguvu akitangulia. Ninaweza kumwona, kwa namna fulani ni mtu mrefu, mkubwa, mwenye mabega yaliyonyooka, mwenye umri wa kama miaka sitini na mitano, akitembea na fimbo mkononi mwake. Huyo hapana budi alikuwa ndiye

yule tunayemwita, Yeye aliyemwita, “Simoni,” na akampa jina lingine la *Petro*, ambalo linamaanisha “kukiri,” ama “jiwe dogo.”

186 Nyuma, watu kumi na wawili wamemzunguka. Watu wakijitokeza mbio, wapate kumgusa yu—yule Rabi alipokuwa anapita. Ninaweza kuwasikia wakisema, “Msimguse Rabi. Alikuwa amechoka. Amehubiri usiku kucha. Nguvu zimemtoka. Amepwelewa na sauti, kutokana na kuzungumza. Msimguse Bwana wetu. Hana budi kushuka aende sasa. Hana budi kupata chakula chake cha mchana. Ni wakati wake wa kula. Na tafadhalini msimguse. Simameni kando, sivyo, tafadhali, na mumpishe Rabi.”

187 Huyu hapa amesimama. Na wakati Zakayo, maskini mfanyabiashara wetu mdogo wa Yeriko, alipomtupia Yesu jicho kwa mara ya kwanza, alionekana yuko tofauti na mtu ye yote aliyepata kumwona.

188 Hebu na tuchomekee kitu kidogo hapa. Huenda bibi fulani alitokeza na mtoto mchanga. Zakayo anaangalia upande *huu*, aone ni nani. “Loo, ninakumbuka wakati daktari alipokuwa nyumbani hivi majuzi. Nilikuwa nimesimama pale wakati kuhani alipokuwa amesimama pale, pia. Daktari anasema, ‘Mtoto huyo hawezi kuishi. Mwekeni chumbani na mfunge milango yote. Msiruhusu hewa.’ Na hapa hiyo familia shupavu ya dini imesikia juu ya Mtu huyu mwongo, anayejiita Nabii wa Galilaya. Wanakuja hapa, na kumleta yule mtoto mchanga, mbona, hii, sheria ya mji inapaswa kumkamata. Nitahakikisha atashikwa, tutakapokutana, ile halmashauri. Tutaona kama mtu, ambaye angemfuata mshupavu wa jambo fulani wa dini kama huyo, kama asingeweza kushughulikiwa. Hana akili timamu.”

189 Nami ninamwona mtu huyo akitoka akikimbia na kusema, “Nina mtoto anayekufa hapa, bwana. Je! ungemruhusu Nabii amguse? Ninaamini ya kwamba Yeye ni Nabii wa Mungu. Nimemwona kwenye mikutano mingine, nami nimesikia habari Zake, na ninajua.”

“La. Samahani. Kuna wengi sana.”

190 Lakini, baada ya kitambo kidogo, maskini mwanamke yule mdogo anatoka, amemshika mtoto mchanga, na huyo mtoto amekufa. “Hebu mwache tu Yeye amguse. Hivyo tu ndivyo ninavyotaka. Ninamwamini. Ninaamini, kama atamgusa mtoto wangu!”

191 “Hatuwezi hata kidogo kufanya jambo hilo, mama.” Yeye yuko mbali sana nao, hata hivyo, anasimama papo hapo njiani.

Ndipo basi ninaweza kumwona Zakayo akilivuta jani lake na kuchungulia.

Kasema, “Mlete huyo mtoto hapa.”

192 Walipomleta huyo mtoto pale, mwili mdogo tu, ana joto jingi, jingi sana. Wakamfunua nguo alizofunikwa nazo. Anaweka vidole vyake juu yake. Mama yake amesimama pale, akiwa na macho yake mazuri, ya Kiyahudi. Machozi yakitiririka mashavuni mwake. Naye baba yake amesimama pale, ameinua mikono yake hewani, akiamini. Naye anaweka kidole chake juu ya mtoto huyo, na homa ikamwacha. Maskini jamaa huyo akaruka kutoka kwenye mikono ya mama yake akatembea barabarani.

193 Zakayo akabadilisha mawazo yake. "Hapana budi kuna jambo fulani halisi kuhusu Mtu huyu. Lakini, afadhali niwe mwangalifu. Afadhali nishushe jani langu, kusudi asinione. Anakuja kupitia huku."

194 Huwezi kamwe kumtupia Yesu Kristo jicho la unyofu na ubaki vivyo hivyo. Kuna kitu fulani kumhusu Yeye ambacho ni cha tofauti na watu wengine wote. Unapomsikia akizungumza, utakuwa kama wale askari wa kirumi, "Hajanena kamwe mtu ye yote namna hii."

195 Makuhani walizungumza juu ya jambo fulani. Mwanadamu bado ana tabia ile ile. Tunayo hayo siku hizi. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, na akitazamia yale ya mbele atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya sasa hivi. Hiyo ni tabia tu ya mwanadamu. Daima imekuwa ni tabia hiyo.

196 Lakini mwanadamu akimwangalia mara moja tu, Yesu Kristo, kamwe hatakuwa ni mtu yule yule tena, akiweza kumwona Yeye amedhihirishwa.

197 Hiyo ndiyo sababu, unapotiwa muhuri na Roho Mtakatifu, muhuri uko pande zote mbili za karatasi, unapokuja na unapokwenda. Wanaweza kuona huo mwenendo, mazungumzo, Maisha ya Kristo yakiakisiwa katika hilo, katika watu Wake. Hilo lilikuwa ndilo kusudi la kifo, kusudi Kanisa liendeleze kazi Yake. Lakini tumelundikana katika kundi la kila kitu.

198 Sasa tunaona, wakati alipoanza kuendelea, akishuka kwenda barabarani. Zakayo anainua jani lake juu kidogo, anataka kumchungulia vizuri sana anapopita. Sasa amefunikwa kabisa, amejificha vizuri sana. Na baada ya kitambo kidogo, inambidi kuinuka namna *hii*, ili kuangalia. Yesu alikuwa akija moja kwa moja chini yake.

199 Alipokaribia tu kupita hapo, Yesu alisimama, akaangalia juu, kasema, "Zakayo, fanya haraka. Shuka mtini. Ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa ajili ya chakula cha jioni leo." Ni tofauti jinsi gani! Yeye alijua huyo alikuwa ni Nabii ambaye Bwana Mungu alikuwa amemwinua. Hakujua tu kwamba alikuwa mtini, bali alijua jina lake lilikuwa ni nani.

200 Biblia ilisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, tena lachoma kugawanya, mafuta ya mfupa, na Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." "Hapo mwanzo

kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwao. Nasi tulimwona, Mwana pekee wa Baba."

201 Alikuwa hapo, Neno la Mungu, lililodhihirishwa kwa Zakayo huyu. Akashuka chini moja kwa moja kutoka kwenye mti, upesi, kutubu.

202 Ewe Zakayo, mfanyabiashara hapa usiku wa leo, kumbuka, huwezi kujificha chini ya majani ya mtini. Anajua kabisa mahali unapoketi hasa. Anakujua. Anajua kwamba wewe ni nani. Anajua jina lako. Anajua kwa nini uko hapa. Anajua yote kuhusu jambo hilo. Hiyo ni kweli.

203 Na sisi ambao tumekutana Naye, na tunamjua, na tumekuwa wanafunzi Wake, tunajua kile Yeye alicho na yale anayowafanyia watu. Tunajua ya kwamba Yeye anadumu yeye yule.

204 Zakayo alishuka, katika moyo wa toba. Akasema, "Kama . . . Bwana, kama nimemdanganya mtu ye yote, nitamlipa. Nitachukua pesa zangu; nitawapa maskini." Unaona, alikuwa tayari amepata ile Lulu ya thamani kuu. Alikuwa amepata kitu ambacho kilikuwa ni zaidi ya biashara yake. Alikuwa amepata kitu fulani, kile kitu Fulani.

205 Na watu wote hujaribu kufanikisha jambo fulani. Lakini kama ukiupoteza Uzima wa Milele, ufanisi wako wote umekufaidia nini? Hazina kubwa kuliko zote ambayo mwanadamu anaweza kupata ni kuwekwa huru.

206 Kama nilivyosema, katika Agano la Kale, wakati ile seli ya damu ilipopasuliwa kutoka kwa mwana-kondoo, isingeweza kumrudia mwabudu, kwa hiyo alitoka akaenda akiwa na tamaa ile ile ya kutenda dhambi. Lakini katika jambo hili, wakati, kwa imani tukiweka mikono yetu juu ya seli ya Damu iliyopasuliwa pale Kalvari; si seli ya damu ya Kiyahudi, wala haikuwa ni seli ya damu ya Mmataifa. Ilikuwa ni Damu ya Mungu, na hapo ndipo ule Uhai uliotoka hapo unapourudisha Uhai wa Mungu kwetu, ambao ni Uzima wa Milele. Neno la Kiyunani hapo linalotumiwa, *Zoe*, ambalo linamaanisha, "Uzima wa Mungu Mwenyewe," na ndio Uzima ule wenyewe uliokuwa katika Kristo, ambao ulikuwa Mungu.

207 Ule mwili ulikuwa ni Mwanadamu, bila shaka. Lakini Mungu, Muumbaji, Ambaye alimfanya mtu wa kwanza! Alitoka wapi kama Yeye hakumuumba? Mungu, Muumba, bila ya msaada wa cho chote kile, alimuumba Adamu. Mungu, Muumba, alimwumba Mwanadamu, Kristo Yesu, Mwanawe, katika tumbo la uzazi la Mariamu. Naye alikuwa ni Imanueli. Na wakati dhambi . . .

208 Si kwa sababu ilimbidi kufa; aliutoa. Lakini kwa sababu dhambi ilipiga, ule mkuki ulioupasua moyo Wake, ndipo kitu fulani kilitukia. Uzima ulimrudia mwabuduo. Na ni kitu gani? "Ndipo hatuna tena dhamiri ya dhambi," anasema mwandishi

wa Waebrania. “Tamaa ya dhambi imekwisha.” Ndipo, sasa tuko huru.

209 Zakayo; walipomwona Yesu akipanda Golgotha, kusulibishwa.

210 Hapana shaka hata hivyo Ibilisi alikuwa sikuzote amemshuku. Ibilisi alimshuku wakati alipomwona kwa mara ya kwanza, wakati Yeye alipoenda jangwani, baada ya Roho Mtakatifu kushuka juu Yake. Yeye alisema, “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, tuonyeshe mwujiza. Geuza mawe haya yawe mkate.” Ibilisi huyo hajakufa bado. “Nionyeshe mwujiza.”

Yesu akasema, “Imeandikwa, ya kwamba, ‘Mtu hataishi kwa mkate tu.’”

211 Wakati walipomkamata kule uani, lile kundi la Ibilisi, hao askari wa Kirumi, waliifunga mikono Yake kwa nyuma, na kumpiga, wakampiga mgongoni na matete pamoja na mjeledi-mkubwa, hadi wapate kutimiza unabii wa manabii. “Kwa kuwa alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa.” Na wakati alipokuwa akiinama . . .

212 Nao askari wakamfunga tambara kuzunguka kichwa Chake, na kumpiga kichwani kwa tete. Na wakapitishiana mmoja kwa mwingine, na kusema, “Kama wewe ni Nabii, tuambie ni nani aliyekupiga. Tutakuamini.” Hiyo dhihaka, na mate ya askari walevi usoni Mwake!

213 Ibilisi akasema, “Huyo hawezi kuwa Mungu. Huyo hata hawezi kuwa ni nabii. Yeye ni mdanganyifu.” Wakiwa hawajui ya kwamba Maandiko hayana budi kutimizwa.

214 Ndipo tunapomwona akipanda kwenda Kalvari, hebu mwangalieni. Nataka kusanyiko hili lipate ono la Yeye. Hebu na turudi nyuma, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, kwa muda kidogo, na mnipe usikivu wenu. Kuna giza juu ya Yerusalemu. Kwa nini? Dhabihu zimekataliwa na Yehova. Jambo fulani liko karibu kutukia. Wakati hiyo damu inapoteketezwa madhabahuni, Mungu aliikataa. Dhabihu halisi inapanda barabarani. Ninaweza kusikia mgongano wa kitu fulani. Naangalia chini, ule pale msalaba wa kale unaoparuza ukienda, chini ya adhabu ya kifo ya Kirumi, ya Mtu ambaye hakukosa lo lote.

215 Nami ninaweza kumwona maskini mwanamke mmoja akitoka na akikimbilia mbele, na kusema, “Yeye amefanya nini ila kuwaponya wagonjwa wenu na kuwafufua wafu?”

216 Mtu fulani akamchapa kofi usoni, na kusema, “Ungemwamini mwanamke huyo kabla hujamwamini kuhani wako? Toka zako hapa na mtu kama huyu!”

217 Angalia koti Lake. Limejaa madoa madogo-madogo mekundu kila mahali, mgongoni. Wakati akiendelea mbele zaidi

juu ya kile kilima, madoa hayo yanazidi kuwa makubwa zaidi na zaidi. Baada ya kitambo kidogo, yote yanakuwa moja. Kuna kitu kinachomdondokea. Ni kitu gani? Ni Damu Yake. Na msalaba unaburuta alama za miguu za Mwenye Kuubeba.

218 Ninaweza kumwona yule nyuki wa mauti akija pale, akivuma karibu Naye. "Nitampata sasa. Kama alikuwa ni nabii, Yeye ange—Yeye angefanya jambo fulani kule wakati walipomtemea mate usoni. Angalikuwa ni nabii, asingeweza kufanya yale anayofanya sasa. Ninajua ya kwamba nitampata."

219 Unajua, kila nyuki, kila mdudu, ana mwiba ndani yake, na mwiba huo ni kitu kibaya.

220 Na mauti yana mwiba ndani yake. Lakini ilimbidi Mungu kufanyika mwili. Angeweza kumchoma nabii na kumshikilia. Angeweza kumdunga mtu mwenye haki na kumshikilia. Alimdunga Daudi na kumshikilia. Lakini huyu hapa Mungu, naye nyuki wa mauti hajui hilo. Huyu nyuki anatoka katika kuzimu, anavuma karibu Naye. "Nitampata."

221 Lakini wakati nyuki anapodunga mwiba wake ndani vya kutosha, anaung'oa mwiba wake.

222 Na wakati huyo nyuki wa mauti angeweza kudunga mwiba wake ndani ya mwanadamu kama mimi ama wewe, angeweza kuwa salama. Bali kulikuwako na mwi—mwili uliotayarishwa; lakini wakati alipodunga mwiba huo ndani ya Yehova, ule mwili wa Mungu, ulioumbwa, si tamaa fulani ya kujuana kimwili. Wakati alipoudunga mwili huo, alipoteza mwiba wake. Basi, yeye hana mwiba tena.

223 Si ajabu kwamba yule Mtakatifu mkuu Paulo angeweza kusimama, wakati walipokuwa wakijenga mahali fulani pale wapate kukikata kichwa chake. Yeye alisema, "Ee mauti, uko wapi mwiba wako? Kaburi, uko wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Naam.

224 Loo, mara mtu anapoona hilo, mengine yote yanawekwa kwa baadaye. Biashara yako ni jambo la baadaye, mengine yote. La, haijalishi sana. Utakaa hapa kwa muda mfupi tu, bali Hilo ndilo jambo la kwanza. "Itamfaa nini mtu kama akipoteza . . . akiupata ulimwengu wote, na kuipoteza nafsi yake?"

225 Zakayo! Loo, Zakayo! Labda si Rebeka aliyeko nyumbani, anayeomba, lakini labda ni mama ambaye tayari amepita ng'ambo ya pazia. Maombi yake yangali yako kwenye madhabahu ya Mungu. Kama hivyo ndivyo ilivyo, ewe Zakayo, toka nyuma ya hayo majani ya mkuyu usiku wa leo: taji hiyo ya kanuni ya imani ya kimadhehebu unayoshikilia, bila ya Kuzaliwa Upya; kitu hicho fulani unachokishikilia, wala hujapata kuwa na thibitisho lo lote ya kwamba Mungu alikuwa katika jambo hilo. Yeye anajua mahali hasa unapoketi. Kwa nini usifanye hivyo?

Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

226 Mwenyezi Mungu, Yehova mkuu na wa kutisha uliyenguruma kutoka katika Mlima Sinai, hata mpaka watu wakasema, "Acha Musa anene wala si Mungu, la sivyo tutakufa." Nena usiku wa leo, Baba yetu wa Mbinguni, katika rehema na msamaha, ndani ya mioyo ya watu wasiokujua Wewe. Na jalia wajue ya kwamba wakati ndio huu. Ya kwamba, wao labda wanajificha nyuma ya biashara zao. Huenda kukawa na wafanyabiashara wengi hapa, Baba, ambao—ambao kweli hawakujui Wewe. Labda wao ni wafuasi wa kanisa, nasi hatusemi lo lote baya kuhusu jambo hilo. Lakini hawajapata kuzaliwa mara ya pili. Hawajui hasa ni kitu gani.

227 Nasi tunajua ya kwamba hakuna yodi moja ama nukta itakayopita kutoka kwenye Neno Lako. Ulisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Nawe ulisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, kwa maji na kwa Roho, hataingia kamwe katika ule Ufalme." Ninaomba, Baba, ya kwamba utazungumza na mioyo usiku wa leo kwenye wakati uu huu. Jalia wanaume na wanawake wawazie kwa uzito, wakati uu huu, tukijua ya kwamba tunaishi katika saa za mwisho.

228 Israeli wako kwenye nchi ya uenyeji wao, ile kalenda kuu ya Mungu. Wanarudi, wakitafuta kujua, "Masihi yuko wapi?"

229 Tunajua ya kwamba wakati Yusufu alipojitambulisha kwa ndugu zake, kwamba aliwaondosha Mataifa barazani pa ikulu. Mke wake na watoto walikuwa katika jumba la mfalme. Kunapaswa kuwe na kuondoshwa kwa Mataifa, Israeli wapate kutambulishwa. Ndipo utakuja wakati wa kuomboleza na kupiga mayowe na kulia, "Je! ulipata wapi makovu hayo?"

230 Yeye alisema, "Kwenye mikono ya rafiki Yangu. Kutoka kwa marafiki Zangu nimepata makovu haya mkononi Mwangu," katika nyumba ambayo kweli alipaswa kukubalika, wakati atakapojitambulisha kwa Israeli tena.

231 Mungu, wakati Mataifa wanayo nafasi, naomba watubu upesi na waje Kwako.

232 Wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, enyi akina Zakayo, ninawataka mwe waaminifu kweli kwa muda kidogo, na akina Rebeka, pia. Katika maskini Ujumbe huu uliokatikakatika, kama kumekuwako na kitu fulani kilichonena na moyo wako na kusema, "Sijapata kamwe kupokea tukio hilo la—la Roho Mtakatifu, Injili kamili, bali ningetaka kulipata. Ninataka unikumbuke katika maombi, Ndugu Branham. Nitaenda tu kuinua mkono wangu, si kwako, bali kwa Mungu." Na useme, "Niombee." Nami nitamalizia maombi, nikikukumbuka. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe, dazani za mikono.

233 Unasema, "Je! hilo linasaidia cho chote, Ndugu Branham?" Kabisa. "Linasaidia namna gani?"

234 Unaona, sayansi inakwambia ya kwamba huwezi kuinua mkono wako, kwa kweli. Sababu, ni kwa nini? Mvutano wa dunia ungeuvutia mkono wako chini. Bali una roho ya uhai ndani yako. Na uhai huo ulio ndani yako, Uhai mwingine ulikuja kwake na kusema, "Umekosea."

235 Nawe ukavunja kanuni za sayansi, na ukainua mkono huo kuelekea kwa Muumba, na kusema, "Nikumbuke." Atakukumbuka. Kama kweli ulimaanisha jambo hilo, Yeye atakuchukulia kwa neno lako. Mungu akubariki wewe huko nyuma. Mtu mwingine sasa kabla hatujafunga? Nitaenda kutoa maombi mafupi hivi punde, tuombe hivi punde. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mtu mwingine?

236 [Dada fulani katika kusanyiko anayanukuu Maandiko—Mh.] Amina. Juu ya rehema, maskini mjakazi huyu anasimama akiwa chini ya Roho, akiinena ahadi.

237 Waweza—waweza kuinua mkono wako kama hujafanya jambo hilo? Na kusema, "Ninii tu. . ." Hayo tu ndiyo nitakayokuomba kufanya. Inua tu mkono wako, ujitambue kwamba umekosea, na unataka rehema. Nyumba iko wazi. "Kuna Chemchemi katika nyumba ya Daudi, iliyofunguliwa kwa ajili ya dhambi na unajisi." Utaikubali usiku wa leo, mtu mwingine, kabla sasa hatujafunga? Kumekuwako na mikono arobaini, hamsini iliyoinuliwa humu jengoni, ya wanaume na wanawake, vijana kwa wazee, waliinua mikono yao. Vema. Mungu akubariki, bwana. Vema.

Na tuombe.

238 Bwana Yesu, ninaamini ya kwamba mikono hii iliinuliwa katika kilindi kabisa cha uaminifu wa moyo. Unajua makusudi yao. Unajua nia zao za kufanya hivyo. Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba rehema Yako ya Kiungu itakaa juu ya kila mmoja wao. Jalia usiku wa leo uwe ni usiku wa kubadilika. Jalia washuke upesi kutoka kwenye mti wa Ufarisayo wa kujibunia. Jalia washuke upesi kutoka kwenye mti huo, mbele za Yesu Kristo, na kusema, "Bwana, kama nilifanya makosa, niko tayari kuyasahihisha." Na kutoka kwenye chumba hiki kidogo cha dhifa usiku wa leo, Baba, Wewe utaenda nyumbani pamoja nao, pia, na kula pamoja nao, na ubaki pamoja nao maishani mwote na Umilele wote. Je! utatujalia jambo hili, ninapotoa maombi yangu Kwako kwa niaba yao?

239 Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Uliahidi jambo hilo.

240 Na sasa, Bwana Mungu, hawa wametolewa kwa ajili ya kumbukumbu za neema na upendo. Wako mikononi Mwako, wala hakuna mtu anayeweza kuwapokonya. Wakiwa waaminifu na wanyofu moyoni mwao, kukiri kwa uaminifu ambako

wamekiri, ya kwamba wanataka kuacha njia za ulimwengu, washike njia za Mungu, kwa ajili ya maisha yao.

241 Wapokee, Ee Bwana, ninaomba, ninapowaombea, nikisimama mbele ya Kiti Chako kikuu Cheupe cha Enzi. Kwa imani tunasimama pale, tukiangalia kwenye Kiti cha Enzi cha kipusa cha Mungu, pamoja na Dhabihu yenye Damu iliyowekwa mbele Zetu, ikituombea tunapokiri. Wasaidie, Baba. Ninawakabidhi Kwako kama karama za upendo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Amina.

242 Sasa, kila mmoja wenu uliyeinua mkono wako, ninataka kuwaombeni mnifanyie jambo fulani. Ninawatakeni mkutane na baadhi ya wahudumu hawa hapa, na kuwaambia ya kwamba mmemkubali Kristo kama Mwokozi wenu, na mnataka kubatizwa, na mnataka kujazwa na Roho Mtakatifu. Naye Mungu atawajalia hayo.

243 Sasa, nilikuwa nikiwazia jambo lingine, bali hatutakuwa na wakati, kwa maana tunapaswa kufunga mahali hapa mnamo—mnamo dakika tano hivi, bali tu—tunathamini saburi yenu.

244 Na mikono yenu yote iliyoinuliwa, sasa, sikujua tu mahali ilipokuwa, kila mahali tu. Lakini wakati ulipoinua mkono wako, hakika ulimaanisha jambo hilo. Usingeinua mkono wako kwa kufanya hivyo tu. Kama uliuinua kwa kuuinua tu, huo ni unafiki. Inua mkono wako. Kamwe usifanye kitu pasipokufanya hivyo kwa uaminifu kweli kweli. Na unapofanya uamuzi huo, na ndani ya moyo wako unamaanisha ya kwamba umefanya hivyo, basi tembea kwa uaminifu na hilo. Mungu atapendezwa na wewe.

245 Aisee, jambo lingine, je! mlijua kilichompata Zakayo? Mngetaka kujua kilichompata? Yeye alifanyika mwanachama wa Shirika la Wafanyabiashara wa Full Gospel la Yeriko. Hivi wewe hutaki kujiunga, pia?

Zakayo, Yule Mfanyabiashara SWA63-0121
(Zacchaeus, The Businessman)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, tarehe 21 Januari, 1963, kwa ajili ya dhifa ya Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Ramada huko Tucson, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org